TANGAZO LA SERIKALI Na. 51R la tarehe 28/1/2025

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA AJILI YA MRADI WA UJENZI WA MTANDAO WA MAJI KATIKA MIJI YA KILWA MASOKO NA NANYUMBU UNAOTEKELEZWA NA WIZARA YA MAJI KUPITIA KAMPUNI YA AFCONS INFRASTRUCTURES AND VIJETA PROJECTS NA INFRASTRUCTURES JV YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Mtandao wa Maji katika Miji ya Kilwa Masoko na Nanyumbu Unaotekelezwa na Wizara ya Maji Kupitia Kampuni ya Afcons Infrastructures na Vijeta Projects and Infrastructures Jv Ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tangu tarehe 11 Disemba, 2023.

Msamaha

**2.** Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa bidhaa zilizoanishwa katika Jedwali i, zilizoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na Wizara ya Maji au Kampuni ya Afcons Infrastructures and Vijeta Projects and Infrastructures JV kwa ajili ya Mradi wa Maji katika Miji ya Kilwa, Masoko na Nanyumbu unasamehewa.

Masharti

**3.** Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa saruji na bidhaa zitatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata

manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

**4.** Amri hii itafikia ukomo wake tarehe 5 Februari, 2025.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

BIDHAA

| Na. | Maelezo | Kipimo | Kiasi |
|---|---|---|---|
| 1 | Saruji | Kilogram | 6,039,000 |

Dodoma,
4/12/2024

**MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU**
*Waziri wa Fedha*